

# MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



## TAARIFA KWA UMMA

### **KUSITISHA UAGIZAJI, USAMBAZAJI, UUZAJI NA MATUMIZI YA DAWA YA MALARIA YA VIDONGE YENYE JINA LA KIBIASHARA LA METAKELFIN YA 'PFIZER INC. N/Y' INAYOTENGENEZWA NA KIWANDA CHA PHARMACIA & UPJOHN YA ITALIA**

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na.1 ya mwaka 2003. Mamlaka ina jukumu la kudhibiti ubora na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ili kulinda afya za watanzania.

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) inapenda kuutaarifu umma kuwa **imesitisha kwa muda** uagizaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya dawa ya vidonge ya kutibu ugonjwa wa malaria aina ya Metakelfin yenye viambata hai (active ingredients) vya Sulphamethopyrazine 500mg na Pyrimethamine 25mg. Dawa hiyo ijulikanayo kama **“Metakelfin ya Italy”** ipo katika paketi ya ujazo wa vidonge 30.

Uamuzi huu umetokana na Mamlaka kubaini kuwepo hapa nchini kwa dawa hiyo ya **Metakelfin ya Pfizer INC. N/Y inayotengenezwa na kiwanda cha Pharmacia & Upjohn, Italia S.p.A. Ascoli Piceno**, ambayo ni bandia kwa kutokuwa na kiambata hai cha Pyrimethamine na pia dawa nyingine zikiwa na kiwango kidogo cha kiambata hai cha Sulphamethopyrazine kinyume na kifungu namba 59 na 76 cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na.1 ya mwaka 2003.

Njia rahisi ya kutofautisha dawa halisi ya Metakelfin na dawa bandia ni kama ifuatavyo:-

Sn	Maelekezo/maelezo	Dawa halisi	Dawa bandia
1.	Rangi ya paketi ya ndani	Fedha iliyofifia	Fedha inayong'aa
2.	Maandishi katika paketi ya ndani	Lugha iliyotumika ni Kiingereza	Lugha iliyotumika ni Kiingereza na Kifaransa
3.	Namba ya bachi, tarehe ya dawa kutengenezwa na muda wa mwisho wa matumizi ya dawa	Maelezo yameandikwa kwa chapa ( printed )	Maelezo yameandikwa kwa muhuri wa moto (embossed)

Orodha ya bachi ambazo Mamlaka imeishazitambua kuwa na matatizo ni **G894A, G895A, G043A, G035A, E378A na G489A**

Mamlaka inapenda kuwataarifu wamiliki wa maduka yanayojihusisha na biashara ya dawa na hospitali zote kutokuuza au kusambaza dawa hizo kwa lengo la kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa hizo. Wale wote watakaokiuka agizo hili, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Watumishi wote wa sekta ya afya ikiwa ni pamoja na wakaguzi wa dawa mnaombwa kufuatilia kwa karibu suala hili ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki pale inapobidi kwa yeyote atakayebainika kuuza au kusambaza dawa hizo katika maduka ya dawa na hospitali.

Wananchi wote kwa ujumla mnaombwa kutoa taarifa haraka ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa, Ofisi za Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya pindi mnapobaini kuwepo kwa dawa hizi katika soko, au watu wanaojihusisha na biashara ya dawa hizo kinyume na agizo hili.

**Nb:** Agizo hili halihusishi dawa za jamii hii zinazotengenezwa na viwanda vingine

Imetolewa na:

**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Chakula na Dawa**  
**Barabara ya Mandela, Mabibo- external**  
**S.L.P 77150,**  
**Dar es Salaam, Tanzania**  
**Simu: +255 22 2450751/2450512/2452108**  
**Fax: +255 22 2450793**  
**Barua Pepe: [info@tfda.or.tz](mailto:info@tfda.or.tz)**  
**Tovuti: [www.tfda.or.tz](http://www.tfda.or.tz)**